

HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA

(Mawasiliano yote yafanywe kupitia kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya)

MKOA: NJOMBE

Simu +255 - 26 2790120
Fax +255 - 26 2790128
Email : ded@ludewadc.go.tz
Tovuti : www.ludewadc.go.tz
Kumb.Na.LDC/J.10/13/93



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),
S.L.P 19,
Ludewa,

Tarehe: 16/05/2019

TANGAZO:

KWA WANANCHI, WAFANYABIASHARA, MAKAMPUNI NA ASASI MBALIMBALI

**HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA INAKUSUDIA
KUTUNGA SHERIA NDOGO ZIFUATAZO:**

- 1. SHERIA NDOGO ZA (ANWANI ZA MAKAZI NA MISIMBO YA POSTA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA ZA MWAKA 2018**
 - ✓ SHERIA NDOGO HII INATUNGWA KWA AJILI YA KUWEKA, KUTAMBUA, KUFUTA MAJINA YA MITAA, SEHEMU NA BARABARA;
 - ✓ KUTUNZA KUMBUKUMBU ZA MAJINA, NAMBARI ZA MITAA, BARABARA, NYUMBA NA RAMANI;
 - ✓ KUTUNZA NA KULINDA MIUNDOMBINU YOTE YA ANWANI ZA MAKAZI NA MISIMBO YA POSTA; n.k.

Mtu yeyote atakayeshindwa kutekeleza masharti ya sheria ndogo hizi au kuvunja Sheria Ndogo hizi na akikutwa na hatia atatozwa faini isiyoziidi Tshs. 300,000/= au kifungo kisichozidi miezi 12 au vyote kwa pamoja faini na kifungo.

2. SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) (MAREKEBISHO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA ZA MWAKA 2018

- a. SHERIA NDOGO HIZI ZITASOMWA PAMOJA NA SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA ZA MWAKA 2017;
- b. SHERIA NDOGO HIZI ZINALENGA KUFUTA, KUONGEZA NA KUPUNGUZA BAADHI YA VIWANGO VYA USHURU WA TOZO MBALIMBALI ZA HALMASHAURI.

Mtu yeyote atakayeshindwa kutekeleza masharti ya sheria ndogo hizi au kuvunja Sheria Ndogo hizi na akikutwa na hatia atatozwa faini isiyopungua Tshs. 200,000/= na isiyozidi Tshs.1,000,000/= au kifungo kisichopungua miezi 12 au kisichozidi miezi 24 au vyote kwa pamoja faini na kifungo

3. KANUNI ZA KUDUMU (MAREKEBISHO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA ZA MWAKA 2018.

- ✓ Kanuni hizi za kudumu zitasomwa pamoja na Kanuni za Kudumu za Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa za mwaka 2014.

TUNAKARIBISHA MAONI AU MAPENDEKEZO KATIKA SHERIA NDOGO NA HIZO, MAONI HAYO YALETWE NDANI YA SIKU THELATHINI (SIKU 30) KUTOKA TAREHE YA TANGAZO HILI, HII NI KWA MUJIBU WA SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA) [SURA YA 287, KIFUNGU CHA 155(1).

KWA MAELEZO ZAIDI, NAKALA ZA SHERIA NDOGO HIZI ZINAPATIKANA OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA LUDEWA (KITENGO CHA SHERIA)

Limetolewa na;



THOMAS KIOWI
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
LUDEWA

Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya
Ludewa